# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI

### TANGAZO LA MWALIKO KWA TAASISI NA ASASI ZA KIRAIA ZENYE NIA YA KUTOA ELIMU YA MPIGA KURA KATIKA UCHAGUZI MDOGO WA UBUNGE JIMBO LA KWAHANI

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inatarajia kuendesha uchaguzi mdogo wa Ubunge katika Jimbo la Kwahani lililopo Wilaya ya Mjini, Mkoa wa Mjini Magharibi, Zanzibar. Uchaguzi huo utafanyika siku ya Jumamosi tarehe 08 Juni, 2024.

Kwa mujibu wa kifungu cha 10(1)(g) na (h) cha Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi Na. 2 ya Mwaka 2024, Tume ina wajibu wa kutoa elimu ya mpiga kura nchini, kuratibu na kusimamia taasisi na asasi za kiraia zinazotoa elimu hiyo.

Hivyo, kupitia tangazo hili, Tume inakaribisha maombi kutoka taasisi na asasi za kiraia nchini zenye nia ya kutoa elimu ya mpiga kura katika uchaguzi mdogo wa Ubunge Jimbo la Kwahani.

Taasisi na asasi za kiraia zenye nia ya kutoa elimu ya mpiga kura zinatakiwa kuwasilisha maombi yao kwa njia ya barua pepe: ***info@inec.go.tz* au *uchaguzi@inec.go.tz***. Maombi hayo yatapokelewa kuanzia tarehe 02 hadi tarehe 07 Mei, 2024.

Barua ya maombi inatakiwa kuainisha mambo yafuatayo kuhusu taasisi au asasi husika:-

i. iwe imesajiliwa kwa mujibu wa Sheria za Tanzania;

ii. iwe imefanya kazi nchini kwa kipindi kisichopungua miezi sita tangu kusajiliwa kwake;



CamScanner

iii. ikiwa taasisi au asasi ya kiraia inahusisha watendaji wa kimataifa, miongoni mwa watendaji wake wakuu, wawili ambao taarifa zao zitawasilishwa wanapaswa wawe Watanzania;

iv. katika utendaji wake, iwe haijahusishwa na uchochezi au kuvuruga amani;

v. iwe na uzoefu wa kutoa elimu ya mpiga kura; na

vi. iwe tayari kujigharamia katika kutoa elimu ya mpiga kura.

Aidha, maombi hayo yanatakiwa kuambatishwa na: -

i. nakala au kivuli cha cheti cha usajili;

ii. nakala au kivuli cha Katiba ya taasisi au asasi ya kiraia;

iii. majina matatu ya viongozi wa juu wa taasisi au asasi ya kiraia;

iv. anuani kamili ya makazi na namba za simu za ofisi na za viongozi wake; na

v. ratiba itakayoonesha tarehe na mahali elimu ya mpiga kura itakapotolewa katika wilaya husika.

**Tume haitahusika na utoaji wa rasilimali fedha au rasilimali nyingine kwa ajili ya kugharamia zoezi la utoaji wa elimu ya mpiga kura kwa taasisi au asasi za kiraia zitakazopewa kibali.**

Limetolewa leo tarehe 02 Mei, 2024 na:

Kailima, R. K
**<u>MKURUGENZI WA UCHAGUZI</u>**



CamScanner